

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA MAMBO YA NDANI YA NCHI

Simu: +255-26-2323189
Barua pepe: ps@moha.go.tz
Tovuti: www.moha.go.tz



MjiwaSerikali - Mtumba,
Mtaawa Habari/Afya,
S.L.P. 2916,
40483 DODOMA.

28 Disemba, 2023

TAARIFA KWA UMMA
ULIPAJI WA ADA YA MWAKA KWA JUMUIYA ZA KIRAIA ZILIZOSAJILIWA
WIZARA YA MAMBO YA NDANI YA NCHI

Ofisi ya Msajili wa Jumuiya, Wizara ya mambo ya Ndani ya Nchi inapenda kuzikumbusha Jumuiya zote za Kidini na zisizokuwa za Kidini kuwa, zinapaswa kulipa Ada ya mwaka na malimbikizo ya ada za miaka ya nyuma kabla ya tarehe 30/06/2024. Ulipaji wa ada ufanyike sambamba na uwasilishaji wa Taarifa za Fedha zilizokaguliwa pamoja na Taarifa ya Utendaji ya mwaka.

Jumuiya ambazo zitashindwa kutekeleza agizo hili katika kipindi husika, zitawajibika kulipa ada pamoja na faini ya kiwango cha asilimia mia moja. Aidha, Jumuiya ambazo hazijatekeleza masharti ya usajili kwa muda mrefu ikiwa ni pamoja na kulipa ada ya mwaka, zitakuwa zimekiuka Sheria ya Jumuiya Sura ya 337, jambo linaloweza kupelekea kufutiwa usajili.

Hivyo, Jumuiya zote za Kiraia zinaagizwa kufika katika Ofisi ya Msajili wa Jumuiya iliyopo Jengo la Kambarage, Ghorofa ya 11 jijini Dodoma au Ofisi ya Msajili wa Jumuiya Kanda ya Mashariki iliyopo katika Jengo la Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi Jijini Dar es salaam, kwa lengo la kupatiwa huduma husika.

Kwa maelezo na msaada zaidi ikiwa ni pamoja na huduma ya kupatiwa namba za malipo, tafadhali piga simu namba 0734 712 744 au 0734 712 745.

Imetolewa na:

Ofisi ya Msajili wa Jumuiya za Kiraia
WIZARA YA MAMBO YA NDANI YA NCHI